

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na:025-2802318/2802137
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA KWA UMMA.
ZIARA YA MHESHIMIWA RAIS WA TANZANIA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN MKOANI
RUKWA KUANZIA TAREHE 15-18 JULAI 2024

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa anawatangazia na kuwajulisha wananchi wote kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, atatembelea Mkoa wa Rukwa kwa ziara rasmi ya kikazi kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 18 Julai 2024.

Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais anatarajia kufanya shughuli zifuatazo:

1. **Kuzindua Miradi:** Mheshimiwa Rais atazindua miradi sita ambayo imekamilika na tayari kwa matumizi ya wananchi.

Miradi hiyo ni:Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nkasi,Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha Lami ya Sumbawanga – Kasanga, Ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Ujenzi wa Chuo cha VETA Sumbawanga na Ujenzi wa ghala/vihenge vya kuhifadhia nafaka NFRA Sumbawanga na Uzinduzi wa Jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kalambo

2. **Kuweka Mawe ya Msingi:** Mheshimiwa Rais ataweka mawe ya msingi kwa miradi ifuatayo: Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga,Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) Kampasi ya Rukwa,Ujenzi wa Barabara kiwango cha Lami ya Kaengesa – Shule ya Sekonadari Seminari ya Kaengesa na ujenzi wa shule ya wasichana ya Sayansi Mkoa wa Rukwa- Laela(Rukwa Girls).
3. **Mkutano ya Hadhara:** Mheshimiwa Rais atafanya Mkutano ya hadhara mmoja siku ya tarehe 17 Julai 2024 kwa ajili ya kuongea na wananchi wa Mkoa wa Rukwa katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga Mjini.

Wananchi mnaombwa kujitokeza na kushiriki kwa wingi katika mapokezi na Kumsikiliza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika kuunga mkono juhudi za maendeleo zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Imetolewa na:
Khadija Dalasia

Khadija Dalasia
Mkuu wa Kitengo Cha Mawasiliano ya Serikali
Mkoa wa Rukwa

11 Julai 2024